

HABARI ZA KAMPUNI KWA UFUPI

KWA UFUPI

# Kantini ya Wafanyakazi

by James Njaala

## Chakula Hatimaye

Uongozi wa KVTC kwa pamoja na uongozi wa chama cha wafanyakazi walianzisha wazo la wafanyakazi kupewa kifungua kinywa na chakula cha mchana. Ujenzi wa kantini uligharimu kiasi cha shillingi milioni sabini na ulikamilika Mei 2019.

## Kwanini Kantini?

Kantini inasaidia sana kuwakutanisha wafanyakazi wote wakati wa mapumziko wakiwa wanapata mlo ulioandaliwa vizuri. Upatikanaji wa chakula KVTC ni muhimu kwani wengi wa wafanyakazi wanatoka mbali na kutembea njia ndefu kufika kazini. Kantini inahakikisha kila mmoja anafurusa ya kupata mlo mara mbili kwa siku.

## Umuhimu wa Kantini

Wafanyakazi wana nufaika kwa kuwa wanaokoa pesa ambayo walikuwa wanatumia kujipatia chakula wakiwa kazini. Sasa wana hela zaidi ya kutumia nyumbani na familia zao. Kuwa na uwezo wa kupata lishe kazini hawatalazimika kuleta chakula cha mchana kilicho andaliwa nyumbani. Hii inasaidia kuongeza ufanisi wa uzalishaji, kuongeza maslahi ya wafanyakazi, kuokoa muda, kuongeza kipato, kuboresha mizanio ya maisha ya kazi na; kuboresha afya na usalama kwa kupunguza ajali zinazosababishwa na kutokula mlo sahihi.

Maandalizi ya chakula yanafanyika katika kantini ya kisasa. Ukaribu wa eneo la kupikia na sehemu ya kulia chakula unahakikisha kuwa chakula kizuri kinatolewa. Sehemu ya uwazi iliyoezekwa inatoa fursa kwa wafanyakazi kupata chakula na hewa mwanana kutoka misitu ya asili inayozunguka eneo hilo iwanda.





*Kantini na eneo la nje la kukaa*

# Mradi wa Misitu ya Asili

Na Demetrius Kweka

Disemba 2018 tuli ripoti changamoto katika kusimamia ardhi yetu ya asili yenye jamii kubwa ya miombo na miti ya kupandwa. Katika robo hii, KVTC imepata ufumbuzi: kwa hiyo imesaini makubaliano na asasi ya MCDI "Uhifadhi wa Mpingo na jitihada za maendeleo" kuandaa ufumbuzi endelevu wa uhifadhi wa eneo la hekta 16,000 zinazokabiliwa na uharibifu mkubwa zaidi katika eneo la Nakafulu bloku C. Mbinu itakayotumika itahakikisha kuvuna kiwango flani kinachostahili kuvunwa kwa uendelevu na kuuzwa bila kuhatarisha uhifadhi wa misitu iliopo. Kiwango kilichovunwa kitagawiwa katika makubaliano maalumu wa kugawana mafao kati ya jamii, KVTC na serikali ya Tanzania. KVTC inaamininjia hii itaboresha ulinzi na uhifadhi katika eneo hili la msitu kwa kuongeza faida (mapato) kwa jamii zinazoizunguka.

Muundo wa MCDI umesifika kwa kutoa manufaa ya msingi kwa jamii na wakati huo huo kuhifadhi wa misitu. KVTC itajifunza uzoefu wa uhifadhi kutoka MCDI, vifaa na utendaji mzuri katika kushirikisha jamii. Huu mfumo utapelekea kutekeleza masharti ya FSC juu ya uhifadhi wa misitu na mpango wa uvunaji wakati taasisi mbili zikinufaika kwa pamoja.

# Kutoka Dawati la Irvine

Na Irvine Kanyemba

Robo yangu ya kwanza katika KVTC imekuwa na shughuli nyingi lakini zenye kufurahisha sana. Tulipata mvua nyingi mwezi wa tano na tulifunga kwa muda shughuli za uvunaji. Mvua ilisimama ghafla kama ilivyoanza na shughuli zimerudi katika hali yake ya kawaida. Viwanda vinne vinavyo nunua magogo kutoka kwetu vimeeanza na vinafanya kazi tena.

Soko la India limetulia kwa kiasi. Kitabu chetu cha oda kinaridhisha. Soko la ndani limeongezeka na tunamatumaini litabaki hivyo. Kuna matumaini ya kuridhisha na yakuvutia huko Rwanda.

Mradi wa usimamizi wa misitu ya asili umeanza. Tunamatumaini makubwa na huu mradi ni muundo bunifu kwa usimamizi endelevu wa raslimali ya misitu ya asili na wanajamii. Hii itasaidia kuimarisha mahusiano ya karibu na jamii inayotuzunguka na uongozi wa serikali za mtaa.

Kantini ya wafanyakazi ilifunguliwa mwishoni mwa Mei.Kantini inatoa kifungua kinywa na chakula kwa wafanyakazi 150 kila siku ya kazi. Imepokelewa vizuri nawafanyakazi wote na kwa uhakika itaboresha hamasa ya wafanyakazi na ufanisi wa uzalishaji.

Tunatarajia robo nyingine yenye changamoto zaidi na mvuto.



# Mfuko wa Jamii KVTC

by Kennedy Haule na Demetrius Kweka

Mfuko wa jamii ni njia bunifu ya kuendelea kutoa msaada kwa jamii waliotoa ardhi kwa KVTC kwa misitu na shughuli za uchakataji. Malengo ya mfuko wa jamii ni kusaidia shughuli za maendeleo ya kijamii na kuboresha maisha ya watu kuzunguka eneo la shughuli za KVTC.
Dhana ya mfuko wa jamii ni kwamba kila mwaka KVTC itatoa jumla ya fedha katika mradi ulioteuliwa katika kila Kijiji shiriki. Mfuko wa Jamii ulianza na vijiji 9 katika wilaya mbili na sasa vimeongezeka mpaka 17 katika wilaya tatu.

Pesa inayopatikana kupitia mfuko wa jamii inaingizwa kwenye akaunti ya pamoja na itatolewa tu kwenye mradi ulio idhinishiwa fedha ulio hakikiwa na pande zote mbili. Maeneo ya kipaombele kwa mfuko wa Jamii ni miradi inayohusiana na afya, elimu, upatikanaji wa maji, na raslimali na uendelezaji wa ujuzi unao husiana na maendeleo ya kiuchumi.

## Umuhimu

Jumla ya shillingi za Kitanzania 871,885,890 (kiasi cha US$ 511,634) kimelipwa kupitia program ya Mfuko wa Jamii kuanzia 2004. Matumizi makubwa ya mfuko wa jamii yalienda kufadhili shule na miradi shirikishi ya shule.

## Ukaguzi na Udhibiti

Kama sehemu ya udhibiti na usimamizi wa miradi ya jamii inayotumia mfuko wa jamiii inawakilishwa kwenye mkutano wa ushauri wa wadau wote.

KVTC inashiriki kwenye mkutano wa hadhara kama sehemu ya mara kwa mara kufuailia utekelezaji wa miradi na inatoa fedha baada ya kuridhika na maendeleo ya mradi

Notisi bodi ya Kijiji vilevile katika kila Kijiji shiriki itaonyesha mradi unao endelea kwa kutumia mfuko wa jamii. Ilikubalika kuwa mfuko wa jamii kukaguliwa na mkaguzi wa serikali za mtaa na taarifa ziletwe KVTC.



*KVTC's Nakafulu Plantation on Google Earth showing the loss of forest cover around the FMU.*

## MIKATABA YA KIJIJI-NYENZO YA KULINDA MSITU

Kwa wastani KVTC inatumia zaidi shillingi TZS million 100 kila mwaka kwa uhifadhi wa misitu kupitia mkataba wa Kijiji. Hizi tarakimu zina imarisha dhana ya kujitoa KVTC kushirikisha jamii katika shughuli zake. Hata hivyo uvamizi mkubwa unafanyika na bila msaada wa mamlaka husika KVTC haiwezi kufanikiwa.

Tunapenda kushukuru uungaji mkono kutoka kwa viongozi wa wilaya katika kuleta uelewa kwa wafugaji na wavamizi wengine juu ya umuhimu wa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi' katika mfululizo wa mikutano iliyofanyika hivi karibuni ikiandaliwa na KVTC.

## SIKILIZA RADIO MITIKI

**RADIO MITIKI**

Sikiliza Radio Pambazuko 89.5FM

Kila Ijumaa saa moja na nusu jioni na kurudiwa Jumamosi saa moja na nusu asubuhi

## WASILIANA NASI

WASILIANA NASI AU TEMBELEA TOVUTI:
kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

S.LP 655, Ifakara, TZ

S.L.P 12452, Dar es Salaam, TZ